

Pambazuko

Toleo Namba 31

Jumatatu Machi 20-26, 2023

Walioficha fedha nje matumbo joto



Uk.10

● Waanza kuhojiwa, wamtupia zigo Magufuli

Tumuombee msamaha Magufuli

**Zitto awaza kifo,
kumrithisha
chama Ado** Uk.6

**Raila Odinga kupima
'pumzi' ya Ruto leo**
Uk.7

Hongera
Rais
Samia.



MFUMI WA TAIFA

Hakika miaka miwili inoitimu jina tangu Tanzania ifumwe uguzi na Rais Samia Saluhu Hassan, haada ya miaka mitano iliyotumbukiza taifa kwenye ramani ya uonevu, mateso na kuminywa kwa demokrasi na uhuru wa vyombo vya habari.

Akante Rais Samia kwe kuwa mfumi wa kuziba maruu na kuanza kutibi makovu ambayo wananchi wanaomba yasirudie tena Tanzania.

JISAJILI HAPA: Andika neno **HABARI** na tuma kwenye namba hii ya WhatsApp - 0744 768263 kupata gazeti bure

Tahariri

Iundwe kurugenzi huru ya kuchunguza Polisi

SIFA za Jeshi la Polisi Tanzania zimekuwa zikibadilikabadiilika kila mara kutegemea nani ni mkuu wa nchi na zaidi sana nani ni Inspekta Jenerali (IGP) kwa wakati huo.

Hakuna siri hata kidogo kwamba kila IGP anakuwa na zama zake; wapo waliofanya kazi vizuri - bila kujiingiza kwenye mtungo wa majambazi, wauza dawa za kulevyu, majangili na hata wanyang'anyi wengine, na hata mafisadi.

Teleweke kwamba wapo baadhi ya wakuu wa jeshi letu la Polisi walioamua kujitunga na magenge hayo ya hovyoy kwa ajili ya kupata utajiri haramu - na wa harakaharaka.

Wapo baadhi ya wakuu wa Polisi walioharibu kabisa nidhamu na sifa ya jeshi hilo lenye majukumu makubwa ya kulinda watu na mali zao. Hawa walishiriki kutesa, kubambika kesi na kuamuru wasaidizi wao kupora mali halali za wananchi ilimradi wao wapate kikubwa na neema, kwa kuumiza wengine.

Kunapotokea matukio haya ya hovyoy, ni watendaji wa jeshi hilo hilo ndiyo hupangwa kuchunguza kilichotokea, hatua ambayo, kwa mizania yoyote ile, haiwezi kuwa ya haki hata kidogo.

Hivi inawezekanaje mtuhumiwa akachunguzwa na watuhumiwa wenzake? Kwamba linalotuhumiwa ni jeshi, na wachunguzi wanakuwa wao. Hapa hakuna haki inayoweza kutendeka, isipokuwa ni kufichwa kwa ukweli na watuhumiwa kuachwa huru, hata kama kuna

kila dalili kwamba walitenda uovu.

Ni kutokana na sababu hizo na kuongezeka kwa tuhuma dhidi ya Jeshi la Polisi, sisi katika Pambazuko tunaona wakati umefika sasa kwa Rais wa Jamhuri ya Muungano, Samia Suluhu Hassan kuunda Kurugunzi Huru ya Upelelezi kwa Polisi.

Tunapendekeza kwamba ikiwa Rais Samia ataridhia kuundwa kwa kurugenzi hiyo, iwe ni sehemu ya watendaji walioko ofisini kwake - Ikulu ili kuwepo kwa ufanisi na kuleta matokeo yanayotarajiwa kwa kila uchunguzi unaofanywa dhidi ya Polisi na watendaji wake.

Ni kurugenzi hiyo, ambayo itaundwa na watu weledi, wazalendo na wafia nchi, ambao umma hautakuwa na chembe ya shaka juu ya tabia zao ndani ya utendaji wa kurugenzi hiyo maalum.

Dhamira kuu ya kurugenzi hiyo ni kuwa chombo chenye ufanisi, huru na kisichoegemea upande wowote katika uchunguzi na usimamizi ambacho kinatenda haki na kwa maslahi ya umma, huku kikidumisha viwango vya juu vya uadilifu na ubora wa watendaji wote wa jeshi hilo bila kujali vyeo na dhamana zao.

Haya yakifanyika, nidhamu, haiba na sifa ya jeshi letu la Polisi inaweza kuimarika na kuwa hasa walenzi wa mali na uhai wa Watanzania, kuliko hali ambayo tumekuwa tukiishuhudia mara kwa mara kwa baadhi ya watendaji wa Polisi kuwa watuhumiwa, wakati mwingine - wa makosa makubwa ikiwamo ya mauaji ya raia.

TULIKOTOKA...



Mbunge wa Chato, ambaye baadaye alikuwa Rais wa Tanzania, John Pombe Magufuli (katikati), akiwa na Mbuge wa Bukoba Mjini (kushoto), Mujuni Kataraiya na Mbunge wa Sumve, Richard Ndasa, wakiwa nje ya Ofisi za Bunge, Dodoma. Hii ilikuwa ni mwaka 1995 wakati wa bunge la kwanza la vyama vingi. Magufuli kama ilivyokuwa kwa Ndasa, ni marehemu. Kataraiya kwa sasa anaishi Minnesota, Marekani. (Picha kutoka Maktaba ya Pambazuko).

NUKUU



“Serikali inafanya kila linalowezekana kuwapa elimu, lakini uamuzi wa kuitumia elimu hiyo ni wenu, tambueni kuwa upo mzigo mkubwa sana wa kuongoza hii nchi unawasubiri, someni kwa bidii sana, mpate maarifa na ufahamu mkubwa. Msituangushe” - Benjamin William Mkapa, Rais wa Tanzania (1995 – 2005). Mkapa sasa ni marehemu.

Tafakuri

Tumuombee msamaha Magufuli

Na Dkt. Lyango KIBASE

ASKOFU Daktari Severine Niwemugizi wa Jimbo Katoliki la Rulenge – Ngara, wiki iliyopita, Machi 17, mwaka huu, alisimama kwenye mimbari ndani ya kanisa lake huko Kilimani, Chato, mkoani Geita na kuutangazia umma kwamba wakati umefika sasa wa kumuombee msamaha kwa Mungu, marehemu John Pombe Magufuli.

Magufuli alikuwa Rais wa Tanzania – katika awamu ya tano kuanzia Novemba 5, 2015 hadi alipofariki dunia Machi 17, 2021 kwa ugonjwa wa moyo.

Niwemugizi alitoa rai hiyo, baada ya kutamka kwamba binafsi anamuombee msamaha kwa Mungu kwa dhambi alizotenda wakati wa uhai wake wote; tangu kuzaliwa na hata kufikia utumishi wa umma wa ngazi ya juu kabisa – urais.

Askofu Niwemugizi katika kujenga hoja yake vyema, alinukuu Injili ya Marko – 11: 25-26; Nanyi mnaposimama kusali, sameheni kila mtu aliyewakosea ili Baba yenu wa mbinguni apate kuwasamehe ninyi makosa yenu.” [26 Lakini msipowasamehe wengine, basi makosa mliyofanya ninyi hayatasamehewa na Baba yenu wa mbinguni.]

Niwemugizi alisema hana uhakika kama Magufuli aliomba msamaha wakati akipigania uhai wake, lakini ana uhakika kwamba alikuwa na dhambi kama ambavyo binadamu wengine wanafanya makosa kwa binadamu mwenzao.

Askofu huyo ambaye ni miongoni mwa watu walionyanyaswa na utawala wa Rais Magufuli, kiasi cha kutishwa kwa uraia wake, anakuwa kiongozi wa juu wa taasisi ya dini kuhimiza maombezi ya msamaha, ingawa angeeleweka zaidi kama angetaja baadhi ya makosa makubwa yaliyofanywa kwa miaka zaidi ya mitano.

Niwemugizi anamuombee msamaha Magufuli kwa kuwa yeye anatambua alikosewa naye kuanzia mwaka 2017



Hayati John Pombe Magufuli.

alipotoa kauli kuhusu umuhimu wa kuwa na katiba mpya ili hatua nzuri zinazochukuliwa na serikali zizingatie misingi ya katiba badala ya kutegemea uamuzi wa mtu. Rais Magufuli hakuwa muumini mzuri wa katiba.

Haikuchukua muda mrefu, Idara ya Uhamiaji ikaanza kuhoji uraia wa askofu huyo na pasi yake ya kusafiria ilishikiliwa na idara hiyo kwa muda mrefu. Hata hivyo, baadaye Magufuli huyuhuyu alieleza “kuwaomba” Uhamiaji kumrejeshea.

Kawaida, mtu anapokwenda kuomba msamaha, anatakiwa kufahamu wapi alikosea na alimkosea nani, lakini kwa kuwa anayeombewa msamaha, sasa hana pumzi, ni vyema wengine wayaweke makosa yake; ambayo ama alifanya moja kwa moja, au kwa kutuma wasaidizi wake.

Miongoni mwa makosa makubwa ambayo yanaambatanishwa na utawala wa Rais Magufuli ni unyang’anyi wa mali za watu, kutekwa, kubambikwa kesi za uongo, madai ya kuzongwa kwa maisha na hata uhai wa baadhi ya watu. Na pia kua mazingira ya utengamano na ushirika miongoni mwa wanasiasa wa vyama vya upinzani na chama chake, Chama Cha Mapinduzi (CCM), kiasi cha kujenga uadui, hali ambayo ilikuwa ngeni mno kwa Watanania.

Tuachane na uteuzi wa DC, RC

Na Dkt. Bullet RUHINDA

MACHI 9, mwaka huu, Rais Samia Suluhu Hassan alimteua Sixtus Mapunda kuwa mkuu mpya wa Wilaya ya Sumbawanga akijaza nafasi ya Dkt. Jane Nyamsenda ambaye alitenguliwa.

Nyamsenda ametenguliwa dhamana aliyopewa baada ya siku 36 tu za kukaa ofisini.

Uteuzi na utenguzi wa aina hiyo; hasa kwa nafasi za wakuu wa mikoa (RC) na wilaya (DC), ingawa upo kisheria na kikatiba, haina maana kwamba hauna dosari.

Miongoni mwa dosari za uteuzi katika nafasi hizo ni pamoja na kwamba sifa za kitaaluma za nafasi hizo hazijulikani.

Jenerali Ulimwengu, mchambuzi wa siasa na mwanasheria, aliwahi kusema cheo cha mkuu wa wilaya au mkoa pamoja na unyeti na umuhimu wake, hutegemea mapenzi ya anayeteua.

Akaongeza, cheo hicho kinaweza kushikwa na Profesa wa chuo kikuu au mtu aliyemaliza darasa la saba, kinaweza kushikwa na jenerali wa jeshi au koplo. Kwa maana nyingine, hakuna vigezo vinavyojulikana kwa nafasi hizo.

Kwa sababu nafasi hizo hazigombewi wala kuombwa, zinategemea utashi wa yule anayeteua, yeye ndiye anajua amteue nani na kwa vigezo anavyovijua yeye.

Nafasi za ukuu wa mkoa ama wilaya – ziko zaidi ya 100, haziombwi kwa maombi ya kazi, hakuna anayetuma wasifu (CV) kwa anayegawa nafasi hizo.

Kwa maana hiyo, mteuzi hawezi kuwafahamu vyema wote anaoamua kuwapa nafasi, hata kama wanapitia mchujo ndani ya taasisi zinazomsaidia rais.

Tuchambue mkuu wa wilaya aliyetenguliwa mwezi mmoja baada ya kuteuliwa. Mpaka anatenguliwa ndani ya muda mfupi, maana yake huenda amefanya makosa makubwa ambayo



Sixtus Mapunda

hayastahimiliki.

Inawezekana hata amefanya mambo ambayo yamewaumiza wananchi kiasi cha ofisi ya uteuzi kufanya utenguzi! Lakini, je nani anaweza kumlaumu aliyetenguliwa? Kwanza, hakuomba kazi, pili sifa zake hazikuwekwa hadharani kabla ya uteuzi wake.

Mteule huyo akishateuliwa na kuwekwa ofisini, wananchi hawana la kumfanya endapo atafanya mambo yasiyofaa. Mfano ni baadhi ya wakuu wa mikoa na wilaya katika awamu iliyopita waliofanya mambo ya hovyona wananchi wakakosa la kufanya juu ya, badala yake wakasubiri huruma ya ofisi ya uteuzi.

Endapo kuna makosa yanafanywa na wateule hao kiasi cha kuwaumiza wananchi, wananchi hawana budi kusubiri huruma ya ofisi ya uteuzi, kuchukua hatua.

Ni kutokana na kuteleza huko kwenye sheria na hata katiba, wateuliwa wanaweza “kuboronga” wakijua kuwa wananchi hawana uwezo wa kuwawajibisha, isipokuwa mteuzi.

Mantiki hapa inaeleza kuwa ni wakati muafaka sasa Tanzania kuwa na katiba mpya ambayo itakomesha nafasi hizo kuwa za uteuzi, bali zishindaniwe ndani ya sanduku la kura ama zitangazwe na watu wenye uwezo waombe na kuchambuliwa kabla ya kutangazwa kuwa wakuu wa wilaya ama mikoa.

Habari

Zitto awaza kifo, kumrithisha chama Ado

Na Tryruckia MFINANGA

KIONGOZI wa Chama cha ACT-Wazalendo, Zitto Kabwe, amesema hata kama atafariki dunia leo, ataondoka akiwa na furaha kuu kwa sababu amekiacha chama chake kwenye mikono salama ya “kijana makini.”

“Mimi ni kiongozi wa chama hiki, nina matamano yangu ya kuona nakipeleka hiki chama kwenda kushika dola, lakini Mwenyezi Mungu naye ana mipango yake, inawezekana nisifike huko, maana Mwenyezi Mungu ana mipango yake,” alisema Zitto wakati akihutubia mkutano wa hadhara wiki iliyopita mjini Tunduma, Songwe.

Anayetajwa na Zitto kuweza kushika “mikoba” ya kukivusha chama hicho cha upinzani hadi kushika dola – kuikalia Ikulu, ni Ado Shaibu ambaye sasa ni Katibu Mkuu wa ACT-Wazalendo.

Ado ambaye ni mwanasheria kitaaluma, anatajwa na baadhi ya wachambuzi wa masuala ya siasa za Tanzania kuwa mwanasiasa mwenye “mwendo wa chatu,” asiyepegia kelele nyingi majukwaani, lakini akijua nini anakifanya kuhakikisha chama anachokiongoza kinaimarika siku hadi siku.

Zitto akiendelea kumpa sifa Ado, anaeleza kuwa ana imani kubwa kwamba hata akifariki dunia Ado ataendelea mapambano ambayo ameyaasisi na kuwa atasimamia misingi ya kukimarisha chama hicho, huku akiunganisha wanachama na wananchi wengine kupiunga na ACT – Wazalendo.

“Nikiitwa na Mwenyezi Mungu kwenye nyumba yangu ya milele, nitaenda nikiamini kwamba nimeacha mtu atakayeendelea yale mapambano kama ambavyo, Oliver Tambo alivyomwachia Mandela (Nelson, Rais wa Afrika Kusini – sasa marehemu); kama ambavyo Edward Mondlane alivyomwachia Samora Machel wa Msumbiji, na huyo mtu ni ndugu yenu Ado Shaibu,” aliongeza Zitto.

Zitto aliwaeleza wananchi wa Tunduma



Zitto Kabwe

na Watanzania kwa jumla, kwamba suala la kuanza kujadili kujiunga na ACT-Wazalendo, siyo mjadala tena, kwani chama hicho ndicho pekee kinachoweza kumkwamua Mtanzania na madhila mengi ya maisha na hata siasa zenye maono.

Ado aliyegombea ubunge wa Tunduru Kaskazini katika uchaguzi mkuu wa mwaka 2020, lakini hakufanikiwa baada ya Hassan Zidada wa CCM kuibuka kidedea, amesema siasa za chama chake cha ACT-Wazalendo kinasimama kwenye kupigania ustawi wa jamii.

ACT-Wazalendo kwa sasa kinaelezwa kuwa chama cha tatu kwa ukubwa nchini Tanzania; kikiwa nyuma ya chama tawala CCM na Chama cha Demokrasia na Maendeleo (Chadema). Hata hivyo, ACT kilianzishwa takribani miaka nane iliyopita, na kupanda kwake kumekifanya kiwe mbele ya vyama vingine mashuhuri vilivyowahi kuwa vikubwa kabla yake; NCCR –Mageuzi na Civic United Front (CUF).

ACT - Wazalendo kilipokea wanachama na baadhi ya viongozi wa juu wa chama cha CUF kilichokuwa na mizizi Zanzibar, na sasa kiko ndani ya Serikali ya Umoja wa Kitaifa (SUK) visiwani humo.

Raila kupima ‘pumzi’ ya Ruto leo

**Na Mwandishi WETU
Nairobi**

KIONGOZI wa chama cha upinzani na mwanasiasa mwenye wafuasi wengi nchini Kenya, Raila Odinga, huenda anatanami kupima ubavu wa kisiasa na Rais William Ruto, kupitia nguvu ya umma, baada ya kuitisha mgomo wa kazi na maandamano leo.

Raila, aliyegombea urais wa nchi hiyo mwaka jana – kupitia jumuiiko la vyama la Azimio la Umoja One Kenya, na kubwagwa na Ruto, aliwataka Wakenya, na hasa wafuasi wake, kuacha kwenda kazini ili kushiriki maandamano hayo yaliyopangwa kufanyika Jiji la Nairobi leo.

Kisheria, mwenye dhamana ya kutangaza kuwepo mapumziko ya kazi ni Waziri wa Usalama wa Ndani wa Kenya na siyo mwingine yeyote. Kwenda kinyume ni kuvunja sheria na katiba ya nchi hiyo ya Afrika Mashariki.

Akiendelea na mikutano yake ya kupinga ushindi wa Ruto na chama chake; Kenya Kwanza, Jumanne iliyopita – Machi 14, Raila akiwa Kaunti ya Siaya alisema ushindi wa Ruto ulikuwa wa “magumashi” na kwamba asiruhusiwe kuendelea kuongoza Kenya kwani aliiba kura za mshindi halali ambaye ni yeye.

“Tunatangaza kwamba Jumatatu, Machi 20 itakuwa siku ya mapumziko,” alisema Odinga, baada ya kutakiwa kufanya hivyo na kiongozi wa chama cha NARC Kenya, Martha Karua.

Karua alimweleza Raila kuwatangazia Wakenya siku ya kupumzika ili kutoa nafasi kwa Wakenya kuhudhuria maandamano hayo yanayotarajiwa kuwa makubwa kutokana na upinzani kuwa na wafuasi wengi.

“Tunakuomba kwa unyenyekevu uifanye siku hiyo kuwa ya mapumziko. Hatuwezi kuendelea kukumbatia masuala ya wizi wa kura kila mwaka. Tunataka ukweli ujulikane,” alisema Karua.

Kufuatia ujumbe huo wa Raila, Rais Ruto amejitokeza hadharani



Raila Odinga

kumtahadharisha Raila kuhusu maandamano hayo, kwani anadai huenda yakaleta rabsha na hata kumwaga damu ya watu wasiokuwa na hatia.

Rais Ruto baada ya tangazo hili, amekuwa akisisitiza na kumuonya Raila kwamba “safari hii serikali haitakaa kimya kuona watu wakiporwa mali zao na hata kupoteza maisha, kwani Raila amezoea kuitisha maandamano ambayo husababisha vifo.”

Tayari vyombo vya usalama ya nchi hiyo vimeonekana vikiranda maeneo mengi ya Nairobi, na hasa yale yanayozunguka Ikulu ya nchi hiyo, kwa hofu ya maandamano hayo kuelekea huko na kuleta vurugu.

Mbali na Rais Ruto kumuonya Raila, mwanasheria na mwanazuoni maarufu wa Kenya PLO Lumumba, ameuasa kiongozi huyo wa Azimio la Umoja One Kenya, kusitisha maandamano hayo maramoja, kwani kufanya hivyo ni sawa na uhaini.

Profesa Lumumba jana alinukuriwa akieleza kuwa anaamini maandamano hayo yataleta shida na kuichafua taswira ya amani ya Kenya – kwani lazima kutakuwepo umwagaji wa damu.

Habari

Janga la kubeti lashika kasi

Na Scovy MANASE

IDADI kubwa ya vijana; wa kike na kiume, sasa wamegeuza michezo ya kubashiri washindi wa mpira wa miguu na michezo mingine, kupitia simu za mkononi ama kompyuta, kuwa ajira.

Vijana hawa pamoja na idadi ndogo ya watu wazima, wanaonekana kujaza vyumba vya michezo hiyo ya kamari katika majiji na miji mikubwa, huku Dar es Salaam ikibainika kuongoza kwa idadi ya wahusika. Miji mingine ni Arusha, Dodoma, Bukoba, Mwanza na Singida.

Inaweza kuelezwa kuwa michezo hiyo ya kubahatisha, maarufu kwa jina la kubeti, imewageuza vijana wengi wa mijini kuwa “ndondocho” kwani kila uchao hudamkia kwenye vituo vya kamari hiyo. Pambazuko limebaini kuwa kamari hiyo sasa imewateka watu wa jinsi na rika na kwamba wamekuwa wakiwekeza fedha nyingi kwa ajili ya kujaribu bahati zao za kuvuna fedha.

Hata hivyo, gazeti hili limebaini kuwa idadi kubwa ya wanaowekeza “mitaji” yao, hawarudishi fedha zao na wala hawabahatiki.

Pambazuko linazo taarifa kwamba Tanzania kwa sasa ina zaidi ya vituo 3,400 vya kubeti, huku Jiji la Dar es Salaam, likiwa na vituo vinavyofikia 1,670.

Vituo hivyo, pia vimebainika kuwa na hata wanafunzi wanaoingiza kujaribu bahati zao, huku usimamizi wa vituo hivyo ukiwa hafifu. Hawawezi kuzuia wenye umri chini ya miaka 18 kuingia huko.

“Hawa wanaangalia pesa tu, hawazui hata watoto kucheza, wanaharibu sana vizazi vijavyo, kwani hawa watoto watageuka na kuwa na uraibu mkubwa wa kamari, na huo ndiyo mwisho wao,” analalamika Judith Kamoge, mfanabiashara eneo la Kariakoo, Dar es Salaam, ambaye amekiri kushuhudia watoto wakiingia kubeti.



Mashine ya kamari

Maeneo ambayo yamesheheni vituo hivyo vya kubeti ni mengi, lakini vingi vimebainika kuwepo Magomeni, Kariakoo, Tandika, Manzese na Temeke Mwisho.

Pamoja na Bodi ya Michezo ya Kubahatisha Tanzania (TGB) kuwa na sheria ya kuharamisha watoto kucheza, wala vituo hivyo kuwa jirani na maeneo ya makazi ya watu, bado sheria hii haizingatiwi na wafanyabiashara wa kamari hizo.

Pambazuko limebaini kuwa wamiliki wakubwa wa vituo hivyo ni “wawekezaji” kutoka China, Afrika Kusini na Marekani, ambao wamesajiliwa na serikali kufanya shughuli hizo ambazo zinaweza kuwa na uraibu mkubwa na kuzidisha umasikini.

Watu wanaojishughulisha na kamari pia wanaweza kupata matatizo ya kisaikolojia kama vile msongo wa mawazo, wasiwasi, unyogovu, na hata matatizo ya kiakili kama vile ugonjwa wa akili.

Tayari Katibu Mkuu wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Daniel Chongolo, amewaonya vijana kuacha kubahatisha maisha kwa kuendelea kucheza kamari, badala yake wajifunze ujuzi mbalimbali, ili wajajiri na kukuza uchumi wao.



Na Evarist Chahali
evarist@chahali.com

Mezani kwa Chahali

Lema na mtanziko wa kauli ya bodaboda

KUNA busara moja nilifundishwa kitambo na nimekuwa nikiizingatia sana kwenye maisha yangu. Inasema hivi, “siyo kila tendo sahihi lina matokeo mazuri, kamba ambavyo siyo kila tendo zuri ni sahihi.”

Kuna mifano miwili inayotumika kufafanua kuhusu busara hiyo. Mfano wa kwanza ni mtu mmoja aliyepitisha siku kadhaa bila kupata mlo.

Bahati nzuri akakutana na msamaria mwema akampikia ugali mkubwa na samaki - huyu mtu mwenye njaa akala kwa haraka, lakini baada ya matonge kadhaa akaanguka.

Bila haja ya kufahamu hatma ilikuwaje, kilichotokea hapo kinaendana na busara niliyoitaja awali. Kitendo cha msamaria mwema kumpa chakula mtu mwenye njaa kilikuwa sahihi.

Hata hivyo, matokeo hayakuwa mazuri kwa sababu japo mtu akiwa na njaa anatakiwa apewe chakula, lakini kwa mtu ambaye hajala muda mrefu (hata aliyefunga kutwa nzima) anapaswa kupata kimiminika kama chai au uji kabla ya kula mlo “mgumu” kama ugali.

Mfano wa pili, mtu na mkewe na binti yao mdogo walikuwa ufukweni. Binti akawa anachezea maji ya bahari. Mara likaja wimbi, likamsomba binti huyo. Bahati nzuri, msamaria mwema mwenye uzoefu wa kuogelea, akajitosa kwenye maji kumuokoa binti huyo.

Hata hivyo, isiyokuwa bahati, katika zoezi hilo la uokoaji, chupi ya binti huyo ilisombwa na maji. Lakini, msamaria mwema huyo alipomkabidhi binti kwa wazazi wake, akapatwa na mshangao baada ya wazazi hao “kumgeuzia kibao” kumtaka awapatie chupi ya binti yao.

Kabla hajaeleza kuwa imesombwa na maji, wakamwambia “akome tabia ya kurandaranda kwenye fukwe kuwinda watoto wanookumbwa na tukio kama



Godbless Lema

la binti yao ili yeye apate nafasi ya kuwatomasa anapowaokoa.”

Msamaria mwema aliyefanya uokoaji alifanya kitu sahihi kujitosa majini kumuokoa binti husika, lakini matokeo yake yakawa tofauti na matarajio.

Nimeikumbuka busara hiyo na mifano hiyo husika kufuatia sakata lililojitokeza baada ya kauli ya aliyekuwa mbunge wa Arusha Mjini kwa tiketi ya Chadema, Godbless Lema, kudai kwamba udereva wa bodaboda ni laana.

Lema aliyaongea hayo huko Arusha mara baada ya kurejea kutoka Canada ambako alikuwa kwenye hifadhi ya kisiasa.

Naamini dhamira ya Lema ilikuwa nzuri – kuwatetea vijana kuhusu ajira – lakini uwasilishaji wa ujumbe husika, hususan matumizi ya neno laana, ulikuwa na mushkeli.

Ikimpendeza Lema, afafanue kinagaubaga alichomaanisha na hakika wengi – hasa madereva wa bodaboda, watamuelewa na kuchukua hatua stahili za kutekeleza majukumu yao, ikiwamo umakini wanapokuwa barabarani.

Inawezekana kuwa na shughuli salama ya biashara ya usafiri wa bodaboda na kuifukuza laana anayoiona Lema.

Habari

Walioficha fedha nje matumbo joto

Na Waandishi WETU

MAOFISA waandamizi kutoka Idara ya Usalama wa Taifa (TISS), Kitengo cha Kudhibiti Fedha Haramu (FIU), na idara zingine, wako kazini kuhakikisha fedha zote zilizofichwa nje ya nchi, zinarejeshwa.

Mbali ya kurejeshwa Tanzania, maofisa hao – wakisaidiana na wachunguzi wengine wa Benki Kuu, wamepewa majukumu mengine, ikiwamo kung’amua wahusika, vyanzo vya fedha hizo na pia hatimaye kufikishwa kwenye vyombo vya sheria, hasa mahakama.

Pambazuko limeelezwa kuwa pamoja na kwamba maofisa hao kupewa majukumu kufuatilia fedha zenye kuhisiwa zimepatikana kiharamu – ikiwamo kutakarishwa, ni moja ya majukumu yao, lakini sasa wamejikita kufuatilia kiasi kikubwa cha fedha ambazo hazifahamiki zimefichwa wapi katika kipindi cha miaka mitano iliyopita.

“Sasa kazi yao ni kubwa na ngumu zaidi, baada ya kubainika kuwepo kwa fedha nyingi kutumika bila idhini ya Bunge, fedha kuchotwa Hazina bila maelezo ya kutosha na madai ya kusafirishwa kwa fedha nyingi za kigeni kwenda nje ya nchi bila maelezo ya kutosha,” kimeeleza chanzo kimoja ndani ya serikali kwa Pambazuko.

Pamoja na chanzo hicho kukataa kutajwa gazetini, lakini kimeeleza kwamba kazi ya kufuatilia fedha hizo inafanywa kwa umakini mkubwa na kwamba wahusika wengi wataanza kuhojiwa hivi karibuni ili kutoa maelezo yao.

Tayari Pambazuko limeelezwa na chanzo kingine kwamba wahusika wawili; viongozi waandamizi wa serikali, wamehojiwa, huku mmoja mwingine akipewa waraka wa wito kufika Ofisi za FIU kwa mahojiano kuanzia leo.

Pambazuko limebaini kuwa viongozi hao wawili waliohojiwa ni miongoni

mwa majina yaliyopo kwenye idara hizo nyeti- ambapo walibanwa kwa maswali ili kueleza uhusika wao, kiasi walichoficha, wapi, na nani aliidhinisha kutolewa fedha kutoka wapi?

Wawili hao walihojiwa kuhusu mabilioni ya fedha ambayo yalikusanywa kutoka kwa watuhumiwa wa kesi mbalimbali ambao walikiri makosa yao kwa Mkurugenzi wa Mashitaka Tanzania ili kuwa huru.

Yapo madai kwamba waliokubali kuingia mkataba na serikali ili kumaliza kesi zao kwa kulipa fedha, walifanya hivyo kwa shinikizo. Kwamba walipeva tu mkataba na kutakiwa kusaini bila kukubaliana kiasi wanachoweza kulipa.

Waliojazimishwa kusaini mkataba wa kununua uhuru wao wapo wengi, lakini walioleleza Pambazuko kwamba walifanyiwa hivyo ni pamoja na Erick Kabendera, mwandishi wa habari za uchunguzi ambaye alitekwa, kufichwa na baadaye kubambikwa kesi ya uhujumu uchumi.

Kabendera baada ya kukaa korokoroni kwa miezi saba na baadaye kulipishwa zaidi ya milioni Sh. 200 ili kuwa huru, ameliambia Pambazuko kwamba “nililazimishwa kusaini bila kufanya makubaliano ya kiasi cha kulipa, ingawa sijawahi kutenda wala kushiriki makosa walionyibambikia.”

Kiasi alichobambikwa Kabendera alilipiwa na wasamaria wema ambao waliamini kuwa hakuwa na kosa aliloshitakiwa nalo, bali ni uonevu na ubabe wa watawala kutaka kuzima midomo na kalamu za waandishi na vyombo makini vya habari.

Mtuhumiwa mwingine ambaye alikubaliana na serikali ili awe huru baada ya kulipa sehemu ya Sh. bilioni 26 alizokubali kulipa ni Harbinder Seith Singh.

Huyu alituhumiwa kwa uhujumu uchumi ni utakatishaji fedha, sambamba

Walioficha fedha nje matumbo joto

Inatoka Uk. 10

na James Rugemalila, ambaye alikataa kukubali utaratibu wa kununua uhuru wake, kwani aliadini kuonewa katika kesi hiyo. Wawili hawa walikuwa wanahisa katika kampuni ya kuzalisha umeme ya IPTL. Hivi sasa Rugemalila yuko huru bila kuingia makubaliano hayo. Serikali iliamua kuondoa kesi hiyo mahakamani.

Rais Samia Suluhu Hasssan, akiwa Ikulu ya Chamwino, Dodoma Januari 31, 2023, wakati wa kuzinduliwa kwa Tume ya Kuboresha Haki Jinai, inayoongozwa na Jaji Mkuu (mstaafu) Othman Chande, aliuambia umma wa Watanzania na dunia kwamba kuna fedha nyingi za Tanzania zimefichwa kwenye mabanki huko China.

Pamoja na kwamba hakutaja majina ya wahusika, lakini alikuwa akimaanisha watu waliohusika na kupokea fedha zilizokuwa watuhumiwa

walioingia makubaliano na serikali ili kumaliza kesi zao (Plea Bargain).

Pambazuko limepata taarifa – na bado linafuatilia, kwamba baada ya kiasi kikubwa cha fedha kukusanywa kupitia kwa waliokuwa watuhumiwa, baadhi zilikuwa na akaunti maalum Benki Kuu ya Tanzania (BoT), lakini kiasi kingine kiliingizwa kwenye akaunti binafsi za watu wawili. Inadaiwa kuwa fedha hizi kwenye akaunti binafsi hazikutakiwa kuguswa na mifumo ya kupokea fedha ya serikali.

Watu hao wawili walipofuatwa na Pambazuko ili kuthibitisha ama kukanusha, walishindwa kutoa ushirikiano wa kutosha; mmoja akiuliza –

“wewe nani amekwambia mimi nahusika, kamuulize huyo, huku mwingine akigeuka mbongo na kushutumua waandishi wa Pambazuko – “nyje badala ya kuandika umasikini wa Watanzania na namna ya kujinasua nao, mnakalia majungu, sina jibu.”

Pambazuko halitawataja majina yao kwa sasa kwa kuwa bado gazeti hili lina “kazi nao kubwa” – katika habari hii.

Wawili hao ambao wamehojiwa, inadaiwa kuwa – jibu lao kubwa lilikuwa ni kupokea maelekezo kutoka ngazi za juu kuhusu “mgawanyo” wa fedha hizo kwenye akaunti mbalimbali.

Mmoja anadaiwa kueleza kwamba mawaziri huapa kwa katiba na kueleza kutii amri za Amiri Jeshi Mkuu, ambaye ni Rais wa Tanzania. Katika kipindi cha utaratibu huo wa kupokea fedha kumalizana na watuhumiwa, Rais wa Tanzania alikuwa John Magufuli (sasa marehemu).

Ripoti ya Mdhhibiti na Mkaguzi Mkuu wa Hesabu za Serikali (CAG), ya 2021/2022 inaeleza kutoeleweka ziliko fedha nyingi zilizokusanywa kwenye utaratibu wa serikali “kumalizana na watuhumiwa.”

Pambazuko ambalo ndilo gazeti pekee lenye wabobezi wa kufuatilia fedha za kutakatishwa na kuwa mwanachama wa taasisi za kimataifa za kuchunguza fedha haramu – ikiwamo ICIJ, Marekani, linaendelea kuchunguza huku likiwa limepata mwanga kwamba wizi huu wa fedha zilizofichwa China ni sehemu ndogo ya ufisadi mkubwa uliofanyika katika serikali ya awamu ya tano ukihusisha vigogo ambao wasingeweza kuguswa na chombo chochote cha dola wakati huo.



Muswada wa Habari

Sheria ya Habari yahitaji uzengezi

Na Hamis MZEE

WAHENGA wamekuwa wakieleza kuwa - “mara zote haki hupiganiwa” – ikiwa na maana kwamba kitu chochote chema hakiwafikii waguswa kirahisi, endapo kitu hicho kinatolewa na watawala.

Kupiganiwa katika muktadha huo, hakuna maana ya kukwaruzana ama “kushikana mashati,” bali ushawishi kwa wenye mamlaka au watawala ili waone umuhimu na faida ya kuruhusu kuwepo neema kwa waguswa ambayo haiathiri uwepo na hata utendaji wa serikali.

Hali hiyo ndiyo inajitokeza katika maboresho ya Muswada wa Sheria ya Huduma za Habari (MSA) ambayo imekuwa ikionekana “kupigwa danadana” kila inapokaribia kuingia bungeni ili kupitishwa na baadaye kuwa sheria.

Ileweke kuwa hata kabla ya kufikia hatua ya kufikishwa bungeni, wanahabari na wadau wa sekta hiyo wamekuwa wakivutana na watawala kuhusu namna ya kuboresha baadhi ya vifungu, huku serikali ikionekana “kukamia” kubaki kwa vifungu inavyopigania, huku wadau – hasa waandishi wa habari wenyewe wakiona vina ukakasi.

Ukakasi unaoelezwa na wanahabari, ni kuwepo kwa dalili za kuminywa kwa uhuru wao wa kufanya kazi ikiwa vifungu “vinavyokumbatiwa” na watawala vitapitishwa.

Kufuatia kuwasilishwa ndani ya Bunge la Tanzania kwa muswada wa marekebisho ya sheria mbalimbali ikiwamo ya Huduma ya Sheria ya Habari, Februari, mwaka huu, wanahabari na wadau wa sekta hiyo bado wanakabiliwa na ‘zigo zito’ la kufanya uzengezi kuhakikisha kuwa muswada huo unabeba mapendekezo yao mengi waliyayotoa kuboresha uhuru wa habari na utendaji wao.

Kwanini ni ‘zigo zito’? - Kinyume na matarajio ya wadau, mapendekezo



Waziri Nape Nnauye

ya marekebisho yaliyomo kwenye muswada uliowasilishwa bungeni ni haba kulinganisha na yale ambayo wanahabari na wadau waliwasilisha kwa Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Nape Nnauye katika vikao mbalimbali kujadili maboresho ya Sheria ya Huduma ya Habari (MSA) iliyopitishwa mwaka 2016.

Hata hivyo, kuwasilishwa kwa muswada wenyewe wa maboresho kuligubikwa na mvutano. Wakati wadau wanatarajia muswada huo uwasilishwe kwenye kikao cha Bunge kilichokuwa kikiendelea wakati huo, ikatolewa taarifa kuwa usingewasilishwa kutokana na Bunge kulemewa na shughuli zingine.

Jukwaa la Wahariri Tanzania (TEF) halikuvumilia kauli ya kuahirishwa kuwasilishwa muswada huo, na kuibuka na kauli kali ya kukerwa kwa hatua hiyo.

Serikali kama vile ilikuwa “ikipima joto” kutaka kuona wanahabari watauchukuliaje uamuzi huo wa kuahirisha kuwasilishwa muswada huo, ikabadili gia na kueleza muswada utawasilishwa kutokana na kuahirishwa kuwasilishwa kwa muswada Bima ya Afya kwa wote.

Ingawa wadau awali waliipongeza

Sheria ya Habari yahitaji uzengezi

Inatoka Uk. 12

hatua hiyo ya kuwasilishwa muswada huo wa marekebisho, sasa wana mawazo mchanganyiko hasa kutokana na mapendekezo yao mengi kutozingatiwa katika muswada wa maboresho.

Pia wadau wangependa Muswada huo wa Marekebisho ya Sheria ya Habari ungewasilishwa pekee siyo kujumuishwa na sheria zingine kama ilivyofanyika.

Wadau wanaona kuwa katika mjadala wa muswada huo wa marekebisho ya sheria mbalimbali, huenda masuala ya habari hayatapewa umuhimu na muda wa kutosha na muda mwingi ukatumika katika sheria zingine zilizomo kwenye muswada huo.

Katika mkutano maalum wa kupata mrejesho kutoka kwa wadau kuhusu mapendekezo ya muswada huo wa habari uliofanyika Machi 13,2023 jijini Dar es Salaam, ilielezwa kuwa kati ya mapendekezo 21 ya wadau ni tisa tu ambayo yameingizwa katika maboresho ya sheria hiyo yaliyowasilishwa bungeni na Serikali.

Katika Sheria ya Habari yenye vifungu 66, masuala muhimu kama vile kutaka kuwepo kwa chombo kimoja badala ya kuwa vyombo viwili- Bodi ya Ithibati ya Wanahabari na Baraza Huru la Habari hayakuzingatiwa.

Baadhi ya wazungumzaji katika mkutano huo ulioandaliwa na Baraza la Habari Tanzania (MCT) lililoanzishwa na wadau wa habari kwa dhana ya kujisimamia, walihoji hilo baraza linalotarajiwa kuundwa na serikali kwa Sheria ya Habari litakuwaje huru?

Pamoja na kuwa mapendekezo yaliyoswasilishwa kwenye muswada huc wa marekebisho yanaondoa udhibiti wa ugawaji wa matangazo kwa vyombo vya habari, bado kuna suala muhimu la kuondoa jinai kwa makosa ya utendaji wa kihabari.

Yaliyofanyika kuhusu jinai katika

mapendekezo yaliyowasilishwa kwenye muswada huo wa marekebisho uliosomwa kwa mara ya kwanza bungeni ni kupunguza adhabu – faini na vifungo tu kwa makosa mbalimbali.

Bila shaka kutokana na hali halisi ya muswada uliowasilishwa, wadau na wanahabari wana kazi kubwa ya uzengezi ya kufanya ili kupata sheria iliyo bora.

Pamoja na jitihada zao, matumaini ya kufanikisha azma yao yanategemea zaidi dhamira na utashi wa Rais Samia Suluhu Hassan ambaye tangu ashike hatamu za uongozi, miaka miwili iliyopita amekuwa mwanga na chachu ya maboresho ya kiuchumi, kisiasa na kijamii nchini.

Vyombo vya habari pia vimenufaika alipoamua kuvifungulia vilivyokuwa vimefungiwa chini ya uongozi wa mtangulizi wake, John Magufuli.

Kwa wachambuzi wa masuala ya habari, inashangaza vipi waziri mhusika aliyeahidi hadharani kuhahikisha uhuru wa habari unalindwa kisheria, ameibuka na mapendekezo ya kuboresha Sheria ya Huduma ya Habari yenye vigingi licha ya serikali kuongozwa na rais mwenye upeo na dhamira chanya kuhusu sekta hiyo?



Kitendea kazi cha waandishi wa habari

Watu Maarufu

Ng'wanamalundi: Muujiza ulioshinda wasomi

Na Ibengwe Shileki MAZEGE

TANZANIA ina historia nyingi zenye kuzisimua na hata kufikirisha. Kuna idadi kubwa ya watu wa kale ambao maisha na shughuli zao za kusifika na hata pengine kutisha, bado hazijaandikwa popote hadi leo licha ya kuwa na wasomi wengi.

Hata hivyo, Pambazuko imeamua kuanza kuibua wazawa wa kale wa nchi hii ili kutunza kumbukumbu kwa kizazi cha sasa na hata vingi vijavyo.

Katika makala haya ya Watu Maarufu, tunaanza na mtu mmoja aliyepata umaarufu zadi katika karne ya 18 hadi 19, akiwa amezaliwa na kukulia Kanda ya Ziwa, sasa ikijulikana kuwa eneo la Mkoa wa Mwanza, ambako wakazi wake wengi ni watu wa jamii ya kabila la Wasukuma.

Ng'wanamalundi ni nani?

Jina la Ng'wanamalundi linamtambulisha mtu wa miujiza kutoka Kabila la Wasukuma, ambaye alizaliwa Kijiji cha Ng'wakwibilinga, Wilaya ya Kwimba, mkoani Mwanza mwaka 1892. Baba yake aliitwa Bugomola na mama yake aliitwa Ngolo.

Wazazi hawa wawili hawakujaaliwa kupata watoto kwa muda mrefu. Uzee ulipowakaribia, Mzee Bugomola ambaye alitamani sana kupata mrithi wa mali zake, lakini haikuwa “fungu lake,” kupata mtoto, hivyo kuamua kutafuta njia za kumpata.

Baada ya muda mrefu kupita, Mzee Bugomola na mke wake Ngolo hatimaye wakakubaliana kwenda kwa mganga upande wa mashariki ya kijiji walichokuwa wakiishi ili wapate ufumbuzi wa tatizo lao.

Mganga aliwafunulia habari za ujio wao hata kabla hawajaketi na kuanza kujitelea wenyewe. Mganga akawatengenezea dawa kisha akawaambia kuwa Ngolo atashika mimba na atazaa mtoto wa kiume ambaye atakuja kuwa mashuhuri siku za hapo baadae, lakini haitakuwa



Ng'wanamalundi

bahati kwa baba wa mtoto – Mzee Bugomola, kwamba hataweza kumuona mtoto huyo. Kwamba Bugomola atafariki dunia kabla mtoto hajazaliwa.

Habari hii ilimfurahisha sana Mzee Bugomola pamoja na kwamba aliambiwa atakufa bila kumuona mtoto. Mkewe pia alifurahi kusikia kuwa atashika mimba. Mzee Bugomola hakujali kifo chake sababu hata umri wake ulikuwa umeenda kidogo.

Furaha kubwa kwake ilikuwa ni kumpata mrithi wake. Wawili hao walianza kurejea kijini kwao siku iliyofuata – huku wakiwa na furaha kubwa. Mzee Bugomola hakuweza kuificha furaha yake kila alipokuwa akizungumza jambo. Muda mwingi alionekana ni mwenye tabasamu na vicheko vingi tofauti kabisa na vile watu wavyomzoea kumuona.

Baada ya wiki kadhaa Ngolo alishika mimba. Mimba ilipotimiza miezi mitatu tu, Mzee Bugomola aliaga dunia bila hata kuugua. Ngolo alilazimika kuilea mimba bila baba wa mtoto kuwa karibu na alitunza hadi ilipofikisha miezi tisa.

Siku moja kabla Ngolo hajajifungua mtoto, wingu kubwa lilitanda angani. Mvua kubwa na yenye radi kali ikaanza kunyesha. Mtoto aliyekuwa tumboni akaruka “mruko” usio wa kawaida na kisha ikasikika sauti ya kitoto kutoka tumboni ikisema, “máyu nibyalage” (maneno ya Kisukuma; yaani “mama nizea”).

Itaedelea wiki ijayo...

Pambazuko

**SASA
TUNAPOKEA
MATANGAZO**

**EWE
MFANYABIASHARA
NA MTOA HUDUMA,
ENDAPO UNAHITAJI
KUWAFIKIA WATEJA
WENGI ZAIDI BILA
KUJALI MIPAKA YA ENEO
ULILOPO, TANGAZA
NASI KWA**

Kuwasiliana kupitia: 0744 768 263
au Barua- Pepe; info@pambazuko.tz

Nigeria**Munkari wa uchaguzi wapo****Na Mashirika ya HABARI**

HOFU ilitanda maeneo mengi huchini Nigeria muda mfupi kabla ya kutangazwa kwa matokeo rasmi ya mshindi wa nafasi ya rais wa nchi hiyo kufuatia uchaguzi mkuu uliofanyika Februari 25, mwaka huu.

Hali hii ilitokana na kuzagaa kwa taarifa kwamba chama tawala, All Progressives Congress (APC), kikiongozwa na Rais Mohammed Buhari, kilikuwa kimeanza wizi wa kura ili mgombea wake, Bola Tinubu atangazwe kuwa mshindi.

Dalili za kuzuka kwa vurugu zilishika kasi na kuwa kubwa zaidi baada ya kucheleweshwa kutangazwa kwa mshindi wa nafasi ya urais.

Hata hivyo, pamoja na vyombo vya dola kuwa “macho,” wananchi wa Nigeria, kwenye maeneo yaliyodhaniwa kuibuka vurugu, yalikuwa tulivu na watu wengi walionekana wakiendelea na shughuli zao za kupambana na maisha.

Pamoja na kuwepo maandamano ya amani ya hapa na pale, ya kupinga matokeo hayo, kwa Tume Huru ya Uchaguzi (INEC) kumtangaza Tinubu kuwa mshindi, hakuna vurugu kubwa ambazo zimeripotiwa hadi sasa.

Maelfu ya wafuasi wa Atiku Abubakar wa chama cha People's Democratic Party (PDP), aliyekuwa akiwania kiti cha urais, wamekuwa wakiandamana hadi katika makao makuu ya Tume Huru ya Taifa ya Uchaguzi (INEC) wakiwa na mabango ya kupinga matokeo hayo.

Hadi sasa, vyama vikubwa vya upinzani vinadai uchaguzi huo ulitawaliwa na wizi wa kura, licha ya taasisi za kufuatilia mchakato huo, zinaeleza kuwa ulikuwa huru na haki.

Waandamanaji wengi, wanaonekana wakiwa na mabango yenye maelezo kwamba mgombea Atiku Abubakar alishinda uchaguzi huo kinyume na ilivyotangazwa na tume ya INEC.

“Tuna ushahidi kwamba tulishinda uchaguzi huu. Tunaamini kuwa INEC

**Rais Bola Tinubu**

haikuzingatia masuala kadhaa muhimu katika kuchakata kura halali, kuna kasoro nyingi ambazo zimebebw kumpa ushindi mtu asiyechaguliwa na Wanaigeria,” alinukuriwa Kola Ologbondiyan, mmoja wa viongozi wa kamati ya kampeni ya ushindi ya PDP

Paul Ibe, mshauri wa Abubakar kuhusu vyombo vya habari, alisema; “huu ni uchaguzi mbaya zaidi katika historia yetu ya kidemokrasia, aliyetangazwa hakuwa mshindi, watu wa Nigeria walikuwa wanatafuta kiongozi atakayewaleta kwenye umoja wa kitaifa na baadaye kupanga namna ya kufufua uchumi uliokufa. Huu uchaguzi uligubikwa na wizi ili mgombea asliyeshindwa atangazwe mshindi.”

Maofisa wa INEC wamekuwa wakigoma kuzungumza na waandamanaji kila wanapofika ofisini kwao.

Tume hiyo huru ya uchaguzi, ilimtangaza Tinubu kuwa mshindi kwa kupata kura milioni 8.8 (asilimia 36) huku mpinzani wake mkuu, Atiku Abubakar akipata asilimia 29. Mgombea mwingine aliyekuwa akipewa nafasi ya kuweza kushinda, Peter Obi wa chama cha Labour alipata asilimia 25. Idadi ya wapiga kura walikuwa waliojitokeza walikuwa zaidi kidogo ya milioni 24, huku wenye kujiandikisha wakiwa milioni 87.

Tinubu ni mmoja wa wanasisia matajiri zaidi Nigeria ambaye inaelezwa alitumia kiasi kikubwa cha fedha na rasilimali zingine kujihakikishia ushindi.

Lema asulubiwa kusema ukweli

Na Martin MASESE

KAZI biashara ya kusafirisha abiria kwa pikipiki, maarufu kwa jina la bodaboda, kamwe haiwezi kuwa ajira ya kujivunia kwa vijana wetu tukiwa nchi inayothamini watu wake.

Kabla ya kuendelea na uchambuzi huu, hebu tujiulize, je, dereva wa bodaboda anaweza kupata bima ya afya? Anaingizwa katika mifuko ya hifadhi ya jamii? Anakopesheka katika taasisi rasmi za kifedha? Analipa kodi (direct tax) yoyote? Hii inakuwa vipi ajira?

Kodi za moja kwa moja hulipwa kutoka kwenye mapato ya biashara kwenda mamlaka ya kodi (TRA); kodi ya biashara za kampuni, kodi za wafanyakazi

na hata kodi za zuio. Hizi kodi bodaboda analipa wapi? Halipi.

Vinginevyo, endapo serikali inataka bodaboda waanze kulipa, lazima waanze kwa kurasimisha bodaboda; waanze kulipa kodi zote stahiki ili itambulike rasmi kwenye mifumo ya serikali, ikiwamo kodi.

Viwango vya kodi hii kwa mapato ya watu binafsi huanzia asilimia tisa mpaka kufikia 30 ya kipato au faida katika mauzo. Hata hivyo, kwa asiye raia ya Tanzania huchajwa asilimia 20 ya jumla ya kipato chake. Bodaboda wakifikia viwango hivi, tutaona hiyo ni ajira rasmi.

Sasa bazi, kumezuka zogo mitandaoni na hata kwenye makundi ya mitandao ya kijamii, wahusika wakimshutumu Godbless Lema, mjumbe wa Chama cha Demokrasia na Maemndeleo (Chadema) alipodai kuwa kazi ya bodaboda ni chanzo

kikubwa cha magonjwa vifo, ulemavu na hata umasikini.

Mzizi wa mnyukano huom wa Lema na bodaboda, ulianzishwa na makada wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), wakieleza kwamba kiongozi huyo wa Chadema anadharau na anafitna na vijana wanaojishughulisha kupata kipato.

Ili kukoleza mvurugano, CCM haraka sana wakaacha kuwaita waendesha pikipiki hizo kwa jina lililozoeleka, bali “maofisa usafirishaji.”

Hata hivyo, ieleweke kuwa hakuna Mtanzania ambaye anaweza kuwachukia bodaboda. Hawa ni vijana wetu. Ni Watanzania wenzetu wanaotafuta kipato kama wengine.

Hivi sasa CCM, kupitia baadhi ya ngazi

za serikali, wanaaminisha umma kwamba bodaboda ni ajira rasmi, ingawa hakuna anayejua idadi yao wala hakuna mfumo wa kuwasajili ili kutambua idadi yao.

Kazi ya bodaboda imeua ubunifu na ufundi. Kazi imeongeza kundi la walala hoi. Hata waliokwenda shule wamejificha katika bodaboda. Waliotakiwa kujajiri katika sekta za ufundi na ubunifu, wanakimbilia kwenye bodaboda.

Kazi ya bodaboda ni shughuli ya kimaskini na hatari kwa yeyote anayeshughulika nayo. Unaweza ukabisha kwa sababu wewe ni mmiliki wa bodaboda 20 au muuza duka la vifaa vya pikipiki, lakini ukweli haujifichi. Bodaboda ni hatari.

Kazi ya bodaboda inatumika kuficha udhaifu wa serikali kwa kushindwa kutengeneza ajira katika sekta binafsi.



Bodaboda

Makala

Lema asulubiwa kusema ukweli

Inatoka Uk. 17

Serikali ya CCM imeshindwa kutengeneza mazingira sahihi na wezeshi kwa vijana kujiajiri kwenye sekta binafsi.

Tembelea hospitali zote kubwa katika mikoza mikubwa Tanzania, tazama vijana waliopata ajali za bodaboda, wanavyotibiwa. Ni kichekesho. Hawathaminiwi. Wakifika tu hospitalini ni kukatwa viungo vya mwili. Wanaonekana ni viumbe visivyostahili kuishi.

Nchi yenye kundi kubwa la vijana, kuwatumia kuendesha bodaboda (kwa kuwapa majina mazuri ya kuvutia eti maafisa usafirishaji) bila kuwatumia katika shughuli za ufundi na uzalishaji wa kisekta, ni kujidanganya.

Tunaweza kuogopa kulieleza ukweli mchungu kundi hilo kubwa la bodaboda kwa sababu za kisiasa tu, kwa sababu wanasisia wengi wanahitaji kupigiwa kura hata kwa maneno ya uongo yenye kutiwa nakshi. Wanasisia wengi ni wasaka kura na kula tu.

Kuliko kusherekea kuwa bodaboda ni ajira, ni vyema kuwaeleza watawala kwamba ni heri kuwahimiza na kuwa na mfumo mzuri wa kuhakikisha vijana wenye nguvu, elimu na maarifa wanafunzwa na kuwezesha kuingia kwenye shughuli za kilimo.

Kilimo ndio sekta inayoongoza katika uchumi wa Kenya, ikichangia asilimia 31.5 ya Pato la Taifa na kuchangia mauzo ya nje kwa kiasi kikubwa. Kenya wanauza zaidi chai, mazao ya bustani na kahawa nje ya nchi.

Ingawa kilimo cha mazao ya bustani kinatawaliwa na uzalishaji wa maua yaliyokatwa, mazao mapya yanawakilisha chanzo kikubwa cha fedha za kigeni, na mauzo ya nje yakizalisha dola za Marekani million 330 mwaka 2017.

Kenya inaongoza kwa kuuza maua ya waridi kwa Umoja wa Ulaya (EU) ikiwa na sehemu ya soko ya asilimia 38. Takriban asilimia 50 ya maua yanayouzwa nje ya Kenya huuzwa kupitia minada ya

Uholanzi.

Kila mwaka Tanzania inanunua tani 1,000,000 za ngano kutoka nje ya nchi na kwa mwaka Tanzania inatumia Shilingi trilion 1.3 kuagiza chakula kutoka nje. Mnaona hii ni sawa? Wakati kundi kubwa la uzalishaji mali limetupa kwenye shughuli za bodaboda.

Tanzania ina jumla la eneo lenye ukubwa wa kilimota za mraba 947,303; eneo lenye maji likiwa na asilimia 6.4 na nchi kavu 93.6.

Inaeleza na wataalamu kwamba asilimia 45 ya eneo lote - la Tanzania linafaa kwa kilimo, wakati sasa ndiyo imezidi kidogo asilimia 25 inayortumika kwa shughuli hizo.

Hadi kufikia robo ya nne ya mwaka 2021, shughuli za kilimo zilichangia karibu asilimia 30 ya Pato la Taifa la Tanzania (GDP). Mnamo 2020, sehemu ya hisa ilifikia asilimia 26.9. Kilimo ni moja ya sekta kuu za kiuchumi Tanzania na tangu 2012, mchango wake katika uchumi wa nchi umebaki juu ya asilimia 25.

Wizara ya kilimo inawasaidia wakulima?

Kilimo, ni tegemeo kuu la maisha kwa takribani asilimia 70 ya kaya, kimeendelea kukua polepole. Sekta ya kilimo, inayoundwa na wakulima wadogo, hajanufaika na kasi sawa na sekta nyingine na inahitaji uwekezaji na kisasa

Vijana kwa sasa wanachangia asilimia 30 ya nguvu kazi, hasa katika kilimo. Hii haitoshi. Asilimia 75 ya raia Tanzania ni vijana. Hii nguvu kazi tukiwekeza katika eneo la kilimo, nchi itapata tija kupitia kilimo na vijana watapata ajira na fedha bila athari.

Ni vyema sasa, serikali ikaangalia namna bora ya kuwezesha uwekezaji wa umma na binafsi zaidi katika kilimo. Wananchi wapewe fursa na wawezeshwe mitaji na pembejeo ili wazalishe na serikali iwatafutie masoko ya bidhaa zao.

Tofauti ya mifumo ya kimaadili

Na Darius RUTAZANA

HAPA duniani kuna utitiri wa mifumo ya kimaadili. Kwa mfano, kuna mifumo wa maadili ya Kikristo, Kiislamu, Kibahai, Kikonfuchio, Kibuda, Kiyahudi, na mifumo wa maadili asilia, kila mifumo ukiwa na migawanyiko kadhaa.

Katika ulimwengu wa Ukristo kuna maadili ya Kikatoliki, Kianglikana, Kilutheri, Kisabato, Kipentekoste, na kadhalika. Katika ulimwengu wa Uislamu kuna maadili ya Kisuni na Kishia.

Katika ulimwengu wa kisekulari kuna maadili ya kikomunisti, kijamaa, kidemokrasia, kifalme, maadili asilia katika mtazamo wa Ulaya, maadili asilia katika mtazamo wa Amerika, na maadili asilia katika mtazamo wa Afrika.

Mifumo hii hufanana na kutofautiana kutokana na inavyojibu maswali ya kudumu juu ya maisha ya mtu mmoja mmoja, mazingira yake ya kimaumbile, mazingira yake ya kijamii, na miungano yenye sura ya sababu na matokeo kati ya mambo haya matatu.

Maswali makubwa katika mifumo hii ni saba; kuna maswali ya kimetafizikia, kiepistemolojia, kisemiotika, kimaadili, kimantiki, kitunu, na jinsi ya kutumia majawabu ya maswali haya sita katika

sekta mbalimbali za maisha ya watu.

Swali la kimetafizikia linauliza, “binadamu ni kitu chenye hulka ya namna gani endapo udhati wake utatazama kama mti wenye matawi mbalimbali?”

Swali la kiepistemolojia linauliza, “tunaweza kupataje maarifa kuhusu hulka ya ubinadamu na matawi yake mbalimbali?”

Swali la kisemiotika linauliza, “tunaweza kutumia alama gani tunapowasiliana kuhusu maarifa tuliyo nayo juu ya hulka ya ubinadamu na matawi yake mbalimbali?”

Swali la kitunu linauliza, “maarifa yetu kuhusu hulka ya ubinadamu yanaonyesha kwamba ni tunu zipi zenye mchango chanya kwa ustawi wake na tunu gani zenye mchango hasi kwa ustawi wake?”

Swali la kimaadili linauliza, “maarifa yetu kuhusu hulka ya binadamu yanaonyesha kwamba ni mbinu zipi zenye mchango chanya kwa ustawi wake na mbinu gani zenye mchango hasi kwa ustawi wake?”

Swali la kimantiki linauliza, “tunawezaje kuchuja na kupata kanuni za kimaadili kutokana na maarifa yetu kuhusu hulka ya ubinadamu, lakini bila kuvunja kanuni za kimantiki?”

Na swali la saba linahusu namna ya kutumia majawabu ya maswali haya sita katika sekta mbalimbali za maisha ya watu, kama vile sekta ya elimu, afya, kilimo, ufugaji, biashara, ujenzi, viwanda, siasa, mazingira, ujinsia, ndoa, na sekta baki.

Kwa kuzingatia “uzio wa miundombinu ya kifikra na kinadharia” uliotajwa, katika kurasa zifuatazo, Ada Lovelace anajadili “maadili asilia katika mtazamo wa wazungu.” Fuatilia.



Wanafalsafa wa Wiki

Maadili asilia kwa mtazamo wa wazungu

Na Dkt. Ada LOVELACE

WAZUNGU wa Ulaya ya kale, kama vile Aristotle wa Ugiriki, Marcus Cicero na Thomas Aquinas wa Italia, Hugo Grotius wa Uholanzi, Thomas Hobbes na John Locke wa Uingereza, walitafsiri kanuni za maadili asilia kwa kutumia misamiati ya enzi zao na kuunda nadharia kongwe ya maadili asilia.

Wanafalsafa hawa wamekuwa na majibu mengi kwa kila hatua na hata maadili ya mfumo wa maisha ya mwanadamu. Maono yao, licha ya kuwa ya miaka mingi, bado yanatumika kuakisi mifumo mingi ya maisha katika siasa, utamaduni, uhusiano na mambo mengi yanayofanyika na kutokea duniani.

Kama ilivyo kwa mifumo baki ya kimaadili, tafsiri ya maono na mitazamo yao inatoa majibu kwa maswali makubwa saba.

Katika kufupisha majibu yao hapa chini, msaada wa fikra za wanzuoni wafuatao zitatumika; J. Budziszewski (1997) na kitabu chake, "Written on the Heart: The Case for Natural Law"; Edward Feser (2015) na makala yake, "In Defense of the Perverted Faculty Argument"; pamoja na Melissa Moschella na Robert George (2015) katika makala yao "Natural Law."

Mosi, kuhusu swali la kimetafizikia linalouliza; "binadamu ni kitu chenye hulka ya namna gani endapo udhati wake utatazamwa kama mti wenye matawi mbalimbali," majibu yao ni kama ifuatavyo.

Kwamba, binadamu ni kiumbehai mwenye mwili, akili na utashi; kwamba, mwili wake unavyo viungo mbalimbali, kila kiungo kikiwa na dira asilia ya kibayolojia inayokielekeza namna ya kutekeleza kazi yake; kwamba, dira



Aristotle

asilia za kibayolojia ni kama mishale inaoielekeza akili ya binadamu katika malengo yaliyo na mchango chanya katika ustawi wake.

Kwa hiyo, basi, kwa kuwa ustawi wa binadamu unakuwepo endapo kila kiungo cha mwili kinatekeleza kazi zake kwa ufanisi, hatua ya kwanza katika kutafuta kanuni za kimaadili ni kubaini na kuheshimu dira asilia za kibayolojia zilizo katika viungo vya mwili.

Na hatimaye, kwa kuwa, binadamu wote wana akili, utashi na dira asilia za kibayolojia inafuata kimantiki kwamba, bila kujali jinsia, dini, rangi, utaifa au kabila ya mtu, dira asilia za kibayolojia ni vigezo thabiti vya kutofautisha tabia njema na tabia mbaya.

Pili, kuhusu swali la kipiistemolojia linalouliza, "tunaweza kupataje maarifa kuhusu hukuwa ya binadamu katika matawi yake anwai," majibu yao ni kama ifuatavyo.

Kwamba, dira asilia za kibayolojia

Maadili asilia kwa mtazamo wa wazungu

zinagunduliwa pole pole kutokana na mafunzo rasmi, kama vile, kupitia masomo ya darasani kuhusu bayolojia, kemia na fizikia.

Tatu, kuhusu swali la kisemiotika linalouliza, “tunaweza kutumia alama gani za mawasiliano tunapobadilishana maarifa tuliyo nayo juu ya hulka ya ubinadamu,” majibu yao ni kama ifuatavyo.


Kwamba, misamiati muhimu katika kambi hii ni: viungo vya mwili, kazi za viungi vya mwili, dira asilia za kibayolojia kama zinavyodhihirika kupitia kazi za viungo vya mwili, ustawi wa binadamu, akili na utashi

Nne, kuhusu swali la kitunu linalouliza, “maarifa yetu kuhusu hulka ya binadamu yanaonyesha kwamba ni tunu zipi zenye mchango chanya kwa ustawi wake na tunu gani zenye mchango hasi kwa ustawi wake,” majibu yao ni kama ifuatavyo.

Kitu chochote kinachohusiana na dira asilia ya kibayolojia kama inavyodhihirika kwenye viungo vya mwili ni tunu ya kibinadamu.

Mfano, uwezo wa kuona kwa macho, uwezo wa kisikia kwa masikio, uwezo wa kuonja kwa ulimi, uwezo wa kunusa kwa kutumia pua, uwezo wa kusukuma damu kwa moyo, uwezo wa kuvuta pumzi kwa mapafu, uwezo wa kupokea na kusaga chakula tumboni, uwezo wa kuzaa watoto kwa kutumia jenitalia, uwezo wa kupoza mwili kwa kutoa jasho kupitia vinyweleo, uwezo wa mama kumnyonyesha mtoto wake kwa kutumia matiti yake, na uweo wa kuendelea kuwa hai, na kadhalika.

Tano, kuhusu swali la kimaadili linalouliza, “maarifa yetu kuhusu hulka ya binadamu yanaonyesha kwamba ni mbinu zipi zenye mchango chanya kwa ustawi wake na mbinu gani zenye



Marcus Cicero

mchango hasi kwa ustawi wake,” majibu yao ni kama ifuatavyo.

Kwamba, kila kitendo cha binadamu kinaambatana na malengo ya aina mbili, lengo la mtendaji na lengo la kitendo. Mfano, kulamba asili ili kufaidi utamu wake ni lengo la mtendaji, wakati kazi ya asili kujenga mwili baada ya kulambwa ni lengo la kitendo.

Kwamba, pale lengo la mtendaji na lengo la kitendo vinapotimizwa bila kubatilishana, basi kitendo hicho kitaleta ustawi wa mhusika, na hivyo kizuri kimaadili.

Na kwamba, pale lengo la mtendaji na lengo la kitendo vinapotimizwa kiasi kwamba lengo moja linabatilisha lengo jingine, basi kitendo hicho hakitaleta ustawi wa mhusika, na hivyo kibaya kimaadili.

Wanachosema ni kwamba, kanuni za maumbile kwa ujumla, na kanuni za maumbile ya kibinadamu kwa upekee, ni mwongozo wa matendo yanayopaswa kufanyika na kuepukwa, sio kwa sababu ya mambo yalivyo wa sasa, bali kwa

Wanafalsafa wa Wiki

Maadili asilia kwa mtazamo wa wazungu

Inatoka Uk. 21

sababu ya mambo yanavyopaswa kuwa hapo baadaye, kulingana na dira asilia za kibayolojia, kama zinavyogunduliwa kwa akili ya kibinadamu.

Sita, kuhusu swali la kimantiki linalouliza, “tunawezaje kuchuja na kupata kanuni za kimaadili kutokana na maarifa yetu kuhusu hulka ya binadamu, lakini bila kuvunja kanuni za kimantiki,” majibu yao ni kama ifuatavyo.

Kwamba, dira asilia za kibayolojia zinazopatikana katika viungo vya mwili ni alama asilia za tunu muhimu za kibinadamu; kwamba, kwa hiyo, tunaweza, kuanzia kwenye dira hizo na kupata kanuni za kimaadili moja kwa moja bila kuvunja kanuni za michujo ya kimantiki.


Kwa mfano, kambi hii inafikiri kama ifuatavyo: Kwamba, kwa kuwa kazi ya matiti ya mama ni kunyonyesha mtoto, basi, ni kosa kufanya kitendo chochote kinachositisha kazi hii.

Mfano ni pale mama anayenyonyesha anapokuwa ofisini na matiti yake yakajaa maziwa, hivyo, akaamua kukamua maziwa na kuyamwaga ili kupunguza maumivu.

Na kwamba, kwa kuwa kazi ya vinyweleo vya kwenye ngozi ni kupoza mwili kwa njia ya kutoa jasho, basi, ni kosa kufanya kitendo chochote kinachositisha kazi hii. Mfano ni pale mtu anapotumia pafyumu zinazozuia kutoka kwa jasho (anti-perspirants).

Na saba, kuhusu namna ya kutumia maarifa kutokana na majawabu ya maswali haya sita katika sekta mbalimbali za maisha ya watu.

Kama tukitumia mfano wa sekta ya “afya ya mama na mtoto,” majibu ya kambi hii ni kama ifuatavyo: Kwamba,



Thomas Hobbes

ni kosa kila wakati, kila mahali, na kwa kila mama anayenyonyesha kukamua na kumwaga maziwa yaliyo katika matiti yake, hata kama hakuna uwezekano wa kumpata na kumyonyesha motto wake kwa wakati huo.

Na kama tukitumia mfano wa sekta ya “vinyweleo na kazi yake ya kupoza mwili,” majibu ya kambi hii ni kama ifuatavyo: Kwamba, ni kosa kila wakati, kila mahali, na kwa kila mhusika kutumia pafyumu zinazositisha kazi ta kutoa jasho mwilini.

Mifano hii miwili haina uhalisia. Hii ndio sababu mojawapo iliyoawalazimisha baadhi ya wanafalsafa wa Marekani kutilia mashaka nadharia ya maadili asilia katika mtazamo mkongwe.

Lakini pia, wanafalsafa hawa, walipinga utaratibu wa kufanya mchujo wa kimantiki ili kupata kanuni za maadili kutokana na kanuni za maumbili, yaani dira asilia za kibayolojia. Kwa maoni yao, utaratibu huu ni sawa na kujaribu kuvuna mchicha kutoka kwenye shamba ya bangi.

Wiki ijayo makala ifuatayo itaonyesha jinsi Wamarekani mamboleo walivyotatua matatizo haya mawili.

Lala salama Lokassa ya Mbongo

Na Asha MABRUKI

KIFO kinaendelea “kuvuna” wakongwe wa muziki wa dansi kutoka Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), safari hii kimechukua uhai wa Denis Lokassa Kasiya, maarufu

Kama Lokassa ya Mbongo.

Amefariki dunia akiwa na miaka 77.

Lokassa, ambaye umarufu wake ulishika kasi kuanzia miaka ya mwishoni mwa miaka ya 1970 na kumea hadi 2000, amefariki Jumanne iliyopita – Machi 14 akiwa Marekani ambako iliarifiwa kwamba alikuwa akiendelea na matibabu katika hospitali ya Nashua, New Hampshire.

Mwanamuziki huyo aliyekuwa akitunga, kuimba na kucharaza gita, alihamia Marekani mwaka 1996 na amekuwa akiishi huko hadi umaui ulipomkuta. Pia alikuwa na makazi yake Paris, Ufaransa ambako shughuli zake za muziki zilifahamika zaidi.

Familia yake imenukurwa ikieleza kuwa Lokassa ya Mbongo alifariki dunia baada ya moyo wake kusimama ghafla. Hata hivyo, taarifa zingine zinaeleza alikuwa akisumbuliwa na ugonjwa wa shinikizo la damu kwa muda mrefu.

Mwezi uliopita, mpiga gita maarufu kutoka DRC, Dally

Kimoko – ambaye ni rafiki wa Lokassa, aliliambia Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) kwamba afya ya Lokassa ilikuwa mbaya na kuhimiza mashabiki wa muziki wake kumuombea kwa Mungu ili apone haraka.

“Hali ya afya ya Lokassa ya Mbongo, ni mbaya, hairidhishi hata kidogo, amekuwa akienda na kutoka hospitali mara kwa mara, tumuombe apone haraka ili aendelee na shughuli za kuipa raha dunia,” alinukuriwa Dally.

Lokassa ya Mbongo kabla ya kuanzisha bendi iliyojipatia umaarufu mkubwa kuanzia Ufaransa hadi Afrika, ikiitwa Soukous Stars - ilikoanzishwa 1989, akiwa na miaka 22, mwaka

1968, alijiunga na bendi ya gwiji mwingine wa miondoko ya Kikongo, Tabu Ley Rochereau ambako alidumu miaka 10.

Soukous Stars ilianza Paris, Ufaransa ikiwa inajumuisha wakongwe wengine wa muziki wa Kikongo

wakiwamo; Ngouma Lokito, Dally Kimoko, Yondo Sister, Ballau Canta, Zeil Zitany na Shimita Maletu.

Lokassa ya Mbongo atakumbukwa zaidi kwa nyimbo alizotunga, kuimba na hata kupangilia ala, zikiwamo; Bonne Annee, Monica, Assitou na Marie-Josse.



KAGAME NA MPIRAAAAAA!



Rais wa Rwanda, Paul Kagame ameungana na Rais wa Shirikisho la Soka Duniani (FIFA), Gianni Infantino na magwiji wengine wa kabumbu duniani (hawapo pichani), kucheza mchezo wa kirafiki jijini Kigali wakati wa ufunguzi wa uwanja mpya wa michezo uliopewa jina la Kigali Pele. Katika mchezo huo uliochezwa Jumatano wiki iliyopita, Rais Kagame ambaye timu yake iliishinda kambi ya FIFA kwa mabao 3-2, alikuwa kivutio kikubwa. (Picha utoka Ikulu ya Rwanda).

GAZETI hili huandaliwa na kusambazwa na Chama cha Waandishi wa Habari Tanzania (Tampa). Pambazuko limesajiliwa na Serikali ya Tanzania, kupitia Idara ya Habari (MAELEZO) na kupewa leseni namba - 0000448.

